

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA RUKWA**  
**Anuani ya Simu: "REGCOM"**  
**Simu Na: 025-2802318/2802137**  
**Nukushi. (025) 2802217**  
Barua pepe: ras@rukwa.go.tz



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
1 Barabara ya Mkoani,  
S.L.P. 128,  
55180 Sumbawanga,  
**RUKWA.**

**TAARIFA KWA UMMA**

**TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSH BILIONI 3 ZA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA SHULE YA SEKODARI YA WASICHANA MKOANI RUKWA KUPITIA MRADI WA SEQUIP**

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa inatoa taarifa ya mapokezi ya fedha kiasi cha Tsh 3,000,000,000/= kutoka Serikali kuu ikiwa ni fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule mpya ya sekondari ya wasichana Mkoani Rukwa kupitia mradi wa Sequip katika Kata ya Laela Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga.

Fedha hizo Bilioni 3,000,000,000/= zitatumika kujenga Shule mpya ya Sekondari ya wasichana Mkoani Rukwa ikiwa na Vyumba vya Madarasa 12, Mabweni 8 Jengo la Utawala, Nyumba za walimu 2 na matundu ya vyoo 16, Maabara 4 (Fizikia, Jiografia, kemia na Bailojia), Bwalo Chumba cha Wagonjwa, Uzio, Vichomea Taka na Mantanki ya kuhifadhi maji.

Utekelezaji wa Mradi wa SEQUIP unatarajia kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunza hasa kwa watoto wa kike na hivyo kuongeza kiwango cha elimu. Mkoa wa Rukwa unaendela kuishukuru Serikali ya awamu ya Sita kwa kuendelea kuleta fedha za miradi ya maendeleo na kuboresha Maisha ya wananchi wa Mkoa wa Rukwa

Imetolewa na

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Khadija Dalasia'.

Khadija Dalasia  
**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**  
**Mkoa wa Rukwa**  
**28 Juni 2023**